KWAYA YA MTAKATIFU KIZITO
PAROKIA YA MWENYEHERI ANUARITE MAKUBURI
+255742000089|+255713975788
kmkmakuburi
www.kmkmakuburi.co.tz
stkizitochoir@gmail.com

NITAMWIMBIA BWANA-B.MUKASA

Kiitikio

Nitamwimbia Bwana, Nitamwimbia Bwana kwa maana ametukuka sana, farasi na mpanda farasi amewatupa Baharini x2

Mashairi

1. Bwana ni nguvu ni nguvu zangu, na wimbo wangu, naye amekuwa wokovu wangu, Yeye ni Mungu ni Mungu wangu, nami nitamsifu nami nitamsifu, ni Mungu wa baba baba yangu, nami nitamtukuza nitamtukuza.

2. Bwana ni mtu wa vita Bwana ndilo jina lake, magari ya farao na jeshi lake amewatupa baharini, maakida wake wateule wamezama vilindini kama jiwe.

3. Bwana mkono wako wa kuume, umepata fahari fahari ya uwezo, Bwana mkono wako wa kuume wawasetaseta adui kwa wingi wa ukuu wako, wawaangusha chini wanaokuondokea.

4. Utawaingiza na kuwapanda katika mlima wa urithi wako, (mahali) mahali pale ulipojifanyia ee Bwana ili upakae pale patakatifu ulipopaweka imara Bwana, kwa mikono yako bwana, utatawala milele na milele